

Mkate wa Siku

NENO LA SIKU

Juni 2022

SIKU
30

SIKU 01 - ZABURI 91:2 (SUV)

“Nitasema, BWANA ndiye kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini.”

SIKU 02 - ISAYA 55:12 (BHN)

“mtaongozwa mwende kwa amani. Milima na vilima mbele yenu vitapaza sauti na kuimba, na miti yote mashambani itawapigia makofi.”

SIKU 03 - 2 PETRO 1:3 (NEN)

“Uweza wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe.”

SIKU 04 - YOELI 2:32a (RSUV)

“Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita jina la BWANA ataponywa...”

SIKU 05 - WARUMI 8:11a (ONEN)

“Roho wa Mungu aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu.”

SIKU 06 - ZABURI 73:24a (SUV)

“Unaniongoza kwa shauri lako.”

SIKU 07 - ISAYA 49:16 (BHN)

“Nimekuchora katika viganja vyangu; kuta zako nazona daima mbele yangu.

SIKU 08 - WAAMUZI 2:1b (RSUV)

“Mimi milele sitalivunja hilo agano langu nililoagana nanyi.”

SIKU 09 - MATHAYO 10:30 (SUV)

“lakini ninyi, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote.”

SIKU 10 - SEFANIA 3:17a (BHN)

“Mwenyezi-Mungu, Mungu wako yu pamoja nawe yeye ni shujaa anayekuletea ushindi.”

SIKU 11 - ZABURI 20:4 (NEN)

“Na akujalie haja ya moyo wako, na aifanikishe mipango yako yote.”

SIKU 12 - ISAYA 40:29 (ONEN)

“Huwapa nguvu waliolegea na huongeza nguvu za wadhaifu.”

SIKU 13 - YAKOBO 4:6 (SUV)

“Lakini hutujalia sisi neema iliyozidi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu.”

SIKU 14 - 1 SAMWUELI 16:7b (RSUV)

“maana wanadamu huitazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo.”

SIKU 15 - KUMB. 8:3b (ONEN)

“...mwanadamu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Bwana.”

SIKU 16 - ZABURI 13:6 (SUV)

“Naam, nimwimbie BWANA, Kwa kuwa amenitendea kwa ukarimu.”

SIKU 17 - ISAYA 43:1b (RSUV)

“...Usiogope, maana nimekukomboza; nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu.”

— INAENDELEA UKURASA
UNAOFUATA.

SIKU 18 - 1 WAKORINTHO 15:10a (NEN)

“Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo na neema yake kwangu haikuwa kitu bure.”

SIKU 19 -ZABURI 50:15 (ONEN)

“na uniite siku ya taabu; nami nitakuokoa, nawe utanitukuza.”

SIKU 20 - NEHEMIA 9:8b (SRUV)

“nawe umetimiza ahadi yako kwani u mwenye haki.”

SIKU 21 - AYUBU 9:10 (BHN)

“Ndiye atendaye makuu yasiyoeleweka, mambo ya ajabu yasiyo na idadi.”

SIKU 22 - YOHANA 10:28 (SUV)

“Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe; wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu.”

SIKU 23 -ISAYA 41:18b (NEN)

“nitageuza jangwa kuwa ziwa la maji, na mahali pakavu kuwa vijito vya maji.”

SIKU 24 -ZABURI 141:3 (RSUV)

“Ee BWANA, uweke mlinzi kinywani pangu, Mngojezi mlangoni pa midomo yangu.”

SIKU 25 - MATHAYO 5:9 (BHN)

“Heri wenye kuleta amani, q maana wataitwa watoto wa Mungu.”

SIKU 26 - KUMB. 28:10 (SUV)

“Na mataifa yote ya duniani watakuona umeitwa kwa jina la BWANA, nao watakuwa na hofu kwako.”

SIKU 27 - METHALI 16:7 (NEN)

“Njia za mtu zinapompendeza Bwana, huwafanya hata adui zake waishi naye kwa amani.”

SIKU 28 - YEREMIA 10:7 (SUV)

“Ni nani asiyekucha wewe, Ee mfalme wa mataifa? Maana hii ni sifa yako wewe; kwa kuwa miongoni mwa wenye hekima wote wa mataifa, na katika hali yao ya enzi yote pia, hapana hata mmoja kama wewe.”

SIKU 29 - ZABURI 119:105 (RSUV)

“Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu.”

SIKU 30 - YOSHUA 1:5b (BHN)


“Daima nitakuwa nawe wala sitakuacha kamwe.”

Makala hii imechukuliwa kutoka
www.biblesociety.ca © Haki zote zimeifadhiwa.

Tunawashukuru sana kwa kuungana na sisi kuenza Neno la Mungu hapa Tanzania na duniani kote kwa ujumla.

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>



&



Canadian
Bible Society

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA